

Taasisi ya Afya Ifakara Haifanyi Utafiti Unaohusisha Watumia Kilevi

> Taarifa hii inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii, hususan WhatsApp ni Feki!



Julai 25, 2022, Dar es Salam. Taasisi ya Afya Ifakara inatoa tahadhari kwa umma kuhusiana na taarifa batili (feki) inayosambazwa hii leo kwenye mitandao ya kijamii, hususan WhatsApp, ikisema kuwa Taasisi yetu inatafuta watumiaji kilevi (pombe) ili washiriki kwenye utafiti wa ugonjwa wa malaria huko Kisarawe, Pwani.

Ukweli ni kuwa taarifa hiyo ni feki na inapaswa kupuuzwa. Taasisi yetu haikuhusika kwa namna yoyote ile kwenye utayarishaji wala usambazaji wa taarifa hiyo batili, na kuwa Taasisi yetu haifanyi wala haina mpango wa kufanya utafiti wa aina hiyo wilayani Kisarawe au mahali pengine popote ndani na nje ya Tanzania.

Vile vile, tunapenda kuutaarifu umma kuwa Taasisi yetu hufanya mambo yake, ikiwemo tafiti za sayansi ya afya ya jamii na mifumo yake, kwa kuzingatia weledi na maadili. Hivyo, tunatoa tahadhari kwa umma kuhusu taarifa hiyo na nyingine kama hiyo ambazo zina viashiria na mwelekeo wa kukiuka weledi na maadili ya kitafiti, na ambazo lengo lake ni kuichafua Taasisi yetu.

Aidha, baada ya kujiridhisha kuhusu undani na vyanzo vya taarifa hiyo, Taasisi yetu itavitaarifu vitengo husika kwenye Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kuhusu taarifa hiyo kwa ajili ya kuchukua tahadhari na hatua za kisheria.



Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano,
 Taasisi ya Afya Ifakara,
 #5 Mtaa wa Ifakara Kitalu Namba 463 Mikocheni | Kinondoni, Dar es Salaam
 +255 222 774 756 | communications@ihi.or.tz

info@ihi.or.tz | www.ihi.or.tz

Tawi la Ifakara

Eneo la Mlabani
 S.L.P 53 Ifakara
 Simu: +255232931572

Ofisi ya Dar es Salaam

#5 Mtaa wa Ifakara Kitalu 463 Mikocheni
 S.L.P 78,373 Dar es Salaam
 Simu: +255222774756

Bagamoyo Branch

Ndani ya Hospitali ya Wilaya
 S.L.P 74 Bagamoyo
 Simu: +255232440065